# Orodha ya stadi:Viatu tiba

| Mshiriki wa mafunzo: | Mshauri: | Tarehe: |
|---|---|---|

| Kutimiza vigezo | Maoni ya Mshauri | Ndio | Hapana |
|---|---|---|---|
| **Hatua ya kwanza: Kuchagua** | | | |
| 1. Inakusanya taarifa inayoendeana na viatu tiba kutoka kwa mhusika kwa kutumia fomu ya tathmini; inaanisha watu wanaopaswa kupata viatu tiba. | | | |
| 2. Inaainisha wakati ambapo mtu anapaswa kupata rufaa kwenda kwenye huduma sahihi. | | | |
| 3. Inaainisha kiatu tiba sahihi kwa ajli ya mhusika kma vile kile kinachofunika vidole, kinachoacha kisigino wazi, na vidole wazi. | | | |
| **Hatua ya pili kutafuta kipimo sahihi** | | | |
| 4. Inatafuta kipimo sahihi cha kiatu tiba cha mhusika.<br>• Inahusisha kupima mguu inavyopaswa kufanyika kwa kuchora kuzunguka mguu.<br>• Kutafuta kipimo sahihi cha viatu na kukikagua<br>5. Tathmini kipimo sahihi.<br>• Kagua ngozi ili kuona dalili za matatizo kila anapotembea kwa dakika 5<br>• Ainisha mambo na kipimo cha kiatu tiba kwa mara ya pili. | | | |
| **Hatua ya tatu: Matumizi** | | | |
| 6. Inamfundisha mtu na mtu anayemtunza namna ya kutumia viatu tiba.<br>• Namna ya kuvaa na kuvua kiatu<br>• Namna ya kukagua mguu ili kujua kama kuna dalili za tatizo.<br>• Soksi zinazofaa. | | | |
| 7. Inafundisha mhusika kutunza viatu tiba vyake<br>• Namna ya kuvitunza<br>• Sehemu vinapoweza kufanyiwa marekebisho<br>• Signs that replacement is needed.<br>• Dalili za kwamba vinapaswa kubadilishwa. | | | |
| 8. Kutoa taarifa ya ziada ya kufuatilia | | | |
| **Hatua ya nne: Ufuatiliaji** | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 9. Inahusisha hatua za ufuatiliaji sahihi, kwa kulingana na tathmini kwa mara ya pili kama vile:<br>• Kubadilisha kiatu tiba baada ya muda sahihi.<br>• Kurekebisha kiatu tiba cha sasa<br>• Kutoa mafunzo zaidi.<br>• Mpe rufaa kwenda kwenye huduma nyingine. | | | |
| **Kwa hatua zote nne** | | | |
| 10. Zingatia kutoa huduma salama na inayomlenga mteja.<br>- Msikilize<br>- Mhamasishe kuuliza maswali<br>- Kama itahitajika, hakikisha mtu anayemtunza au mwanafamilia anashirikishwa katika hatua zote.<br>- Pata ridhaa<br>- Muweke katika mkao salama na safi kwa ajili ya kupata huduma zote. | | | |

**Mambo ya kuzingatiwa na Mwezeshaji.**

**Tumia Orodha hii ya stadi kukusaidia:**

- Tathmini namna Washiriki wa Mafunzo wanavyotekeleza stadi za ugawaji wa vifaa tiba na kama:
    - Wanaweza kufanya kugawa viatu tiba kupewa msaada kutoka kwa mtu mwingine, au
    - Wanahitaji mafunzo zaidi ya vitendo na kama ndicho hicho wanachokihitaji, tambua aina ya stadi wanazohitaji kufanyia mazoezi.

**Kumbuka kwamba:**

- Hii Orodha ina Stadi muhimu ambazo ziko kwenye moduli ya TAP.
- Kuna stadi nyingine ambazo ungependa Watoa huduma wako kuwa nazo kulingana na mahitaji ya huduma wanazozitoa. Unaweza kuongeza mambo mengine kwenye Orodha hii kama kwa kufanya hivyo itasaidia zaidi.
- Unaweza kutokuona stadi hizo hapo juu kwenye hatua zote nne kwa mkupuo mmoja, utaweza kuziona hapo baadaye unavyofanya ufuatiliaji.

**Ili kutumia Orodha ya Stadi**:

- Fuatilia kwa karibu namna ambavyo Washiriki wa Mafunzo wanagawa viatu tiba. Hii inaweza kufanyika kwa kufanya igizo (mmoja akiwa Mteja mwingine kama Mtoa huduma) au kufanya igizo na Wateja.
- Hakikisha kuwa zoezi na Wateja linafanyika kwa usalama.
- Andika kwenye fomu kama Mshiriki wa Mafunzo amefanya kila stadi kwa usahihi. Andika maelezo kwenye eneo la kutoa maoni. Hii inaweza kuwa vitu ambavyo Mshiriki wa Mafunzo amefanya vizuri Zaidi au maeneo ambayo anapaswa kuboreshwa Zaidi/anahitaji mafunzo Zaidi.

**Utoaji wa mrejesho kwa Washiriki wa Mafunzo**

- Jadili na Washiriki wa Mafunzo kuhusu mambo uliyoyaona. Wajulishe mambo wanayoyafanya vizuri na maeneo ambayo yanahitaji kuboreshwa.
- Wape nakala ya Orodha ya Stadi iliyokamilika kwa ajili ya wao kuweka kumbukumbu.
- Endelea kutoa mafunzo kwa vitendo na msaada pale unapohitajika na fanya tathmini mara kwa mara ili kuboresha stadi na kujenga hali ya kujiamini.

**Ni wakati gani Mshiriki wa Mafunzo anaweza kugawa viatu tiba bila ya kupata usaidizi?**

- Ili kuafnya kugawa viatu tiba kwa usahihi bila msaada,mshiriki wa mafunzo anapaswa kukamilisha stadi zote kwa usahihi.
- Kumbuka- kutoa mafunzo kwa vitendo na kusimamia ni mchakato endelevu ili kuboresha stadi.